

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**  
**(*Shirika La Magereza*)**  
**(*Kampuni ya Ulinzi Shima*)**



**31 Machi, 2023**

**YAH: TAARIFA KWA UMMA KUHUSU NAFASI ZA MAFUNZO  
YA KAMPUNI YA ULINZI SHIMA.**

Kampuni ya ulinzi Shima Guard ni kampuni tanzu ya Shirika la Magereza (SHIMA) ambayo imesajiriwa kwa mujibu wa sheria za makampuni binafsi tarehe 23/10/2020. Kampuni ya ulinzi Shima inatoa huduma ya ulinzi kwenye taasisi za Serikali pamoja na taasisi binafsi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ulinzi Shima anatangaza nafasi za kujiunga na mafunzo ya Kampuni ya ulinzi Shima Guard yatakayofanyika Dodoma Gereza Isanga.

**1. SIFA ZA WAOMBALI**

- Awe raia wa Tanzania
- Asiwe mlevi
- Awe na umri wa miaka 20 – 45
- Awe hajawahi kuhukumiwa au kuwa na rekodi ya makosa ya jinai
- Awe na elimu ya kuanzia darasa la saba hadi kidato cha sita
- Awe na tabia njema
- Awe anajua kusoma na kuandika Kiswahili au kiingereza kwa ufasaha

- Awe tayari kufanya kazi mahali popote atakapopangiwa mara baada ya kumaliza mafunzo
- Awe amefanya mafunzo ya JKT au Mgambo
- Awe hana rekodi ya matumizi ya dawa za kulevyia
- Awe na akili timamu

## **2. BARUA YA MAOMBI ITUMWE IKIWA NA VIAMBATANISHO VIFUATAVYO**

- Barua ya maombi ikiwa na Passport moja na iwe imegongwa mhuri kama utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa/ kijiji anakotoka muombaji.
- Barua ya wadhamini wawili (02) wenyewe utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa/ kijiji zikiwa na picha za wadhamini na namba zao za simu
- Barua ya utambulisho kutoka kwa mtendaji / mwenyekiti wa Serikali za Mitaa sehemu anapoishi
- Nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) au cha mpiga kura/Namba ya NIDA.
- Form za uthibitisho wa afya kutoka Hospitali ya Serikali

## **3. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI**

Barua ya maombi ya kujiunga na mafunzo ikiwa na namba ya simu ya muombaji ziletwe ofisi ya Shima Guard Makao Makuu Dodoma, Jengo la Uhamiaji na Magereza Mkao Ghorofa ya pili, mkabala na Nyerere Square Kabla ya tarehe 04/04/2023 na wale ambao wapo nje ya Dodoma maombi yatumwe kwenye email ya [shimaguard@prisons.go.tz](mailto:shimaguard@prisons.go.tz).

Tangazo limetolewa na,

**ALLI ABDALLAH UWESSU – SSP  
MKURUGENZI MTENDAJI, KAMPUNI YA ULINZI SHIMA.**

